

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI**

SHULE YA SEKONDARI IHOWANZA
S.L.P 10,
MALANGALI.

Kumb.

Ndg

.....

.....

**1.0 YAH: MAAGIZO NA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA
MWAKA 2021**

Ninayo furaha kubwa kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika Shule hii. Nakupongeza sana kwa kuchaguliwa na nategemea utaitumia nafasi hii ipasavyo ili kujenga historia nzuri ya maisha yako. Ni mategemeo ya shule kuwa uwapo hapa utashirikiana vizuri na walimu, Watumishi wasio walimu na wanafunzi wenzako kufanya kazi za darasani na nje ya darasa. Shule itafungua tarehe **11/01/2021**. Ili kuanza masomo yako kikamilifu na kwa wakati, ukichelewa utaipoteza nafasi hii adimu.

2.0 MAHALI SHULE ILIPO NA NAMNA YA KUFIKA SHULENI

Shule ipo Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Mufindi, Tarafa ya Malangali Kata ya Ihowanza. Ukitokea Mafinga au Makambako kwa kufuata barabara kuu itokayo Dar es salaam kwenda Mbeya, Shuka kituo cha mabasi kiitwacho Mbalamaziwa, hapo utapata usafiri wa kuja Ihowanza sekondari umbali wa kilometa 26 Magharibi mwa mbalamaziwa.

3.0 SARE ZA SHULE

A) WAVULANA

3.1 Shati mbili nyeupe kabisa tetron au Polista, zenye ukosi wa kawaida, Shati moja mikono mifupi na linginge mikono mirefu pamoja na tai mbili, moja nyeusi na nyingine kijani mgomba.

3.2 Suruali mbili, moja rangi ya kijani mgomba na nyeusi moja. Ziwe na rinda na upindo miguuni. Upana wa chini uwe wa inchi 16, mkanda wa kuvalia suruali uwe wa ngozi rangi nyeusi (chuma cha kwenye mkanda kisiwe na urembo na maandishi ya aina yoyote, pia usiwe utambi).

3.3 Viatu vyeusi jozi mbili, visiwe buti, viwe vya kamba. Viatu visivyofungwa na kamba havikubaliki/haviruhusiwi.

3.4 Jozi mbili za soksi nyeusi.

3.5 Fulana moja rangi damu ya mzee (T- shirt) na Sweta nadhifu la kijani lenye V shingoni.

B) WASICHANA

4.1 Shati mbili nyeupe kabisa tetron au Polista, zenye ukosi wa kawaida, Shati moja mikono mifupi na linginge mikono mirefu pamoja na tai mbili, moja nyeusi na moja kijani mgomba.

4.2 Sketi mbili ndefu mshono wa lindabox zinazofunika soks, moja rangi ya kijani mgomba na nyeusi moja.

5.0 CHAKULA NA VIFAA

5.1 Mahindi yaliyokobolewa Debe moja (20kg) kwaajili ya chakula cha mchana kwa nusu muhula.

5.2 maharage kilo 5 kwa nusu muhula

5.3 Fedha shilingi 5000/= kwa ajili ya viungo na malipo ya mpishi, kwa nusu mwaka.

5.4 Kontena/sahani, Kikombe na Kijiko.

6.0 VIFAA VYA TAALUMA

- 6.1 Uje na daftari kubwa (Counter books) zisizopungua 09, mathematical set na peni za kutosha.
- 6.2 Spring file moja kwa ajili ya kutunzia maendeleo ya mwanao.
- 6.3 Daftari ndogo 09 (msomi) kwa ajili ya mazoezi.
- 6.4 Kamusi ya kiingereza na kiswahili

7.0 VIFAA VYA USAFI

- 7.1 Jembe jipya lenye mpini.
- 7.2 Ndoo ndogo ya lita kumi.
- 7.3 Mfagio (chelewa) mmoja

8.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

8.1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978.

Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

- (a) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za shule ndani na nje ya shule ni muhimu
- (b) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation)
- (c) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
- (f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- (g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- (h) **MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUMILIKI AU KUTUMIA SIMU KIPINDI CHOTE AWAPO SHULENI.**

9.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZA SHULENI.

1. Wizi
2. Uasherati, Ubakaji na Ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya. kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli nakadhalika.
4. Uvutaji bangi na sigara
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kupata mimba/kusababisha mimba
10. Kulawiti
11. Utoro
12. Kutofanya mazoezi au mitihani ya masomo na kutega vipindi
13. Kiburi na ukaidi
14. Kugoma/kuchochea na kuongoza mgomo
15. Kukataa adhabu kwa makusudi
16. Kumiliki/kutumia simu shuleni

TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA UTAPOKELEWA SHULENI BAADA YA KUTIMIZA YOTE ULIYOAGIZWA. NAKUTAKIA SAFARI NJEMA, KARIBU SANA IHOWANZA SEKONDARI.

.....
ABEL .E. KIHONGOSI (+255753538174)
MKUU WA SHULE